

13C-Al-Waqf At-Taamm (Kisimamo Kilichokamilika)

i. **الْوَقْفُ التَّامُّ Al-Waqf At-Taamm - Kisimamo Kilichokamilika**

Kusimama katika neno la Qur-aan ambako kauli imekamilika maana yake, na wala hayana uhusiano wowote ule na yanayofuatia; uhusiano huo uwe wa kimaana au wa kilugha. Mfano kila inapomalizika Suwrah ya Qur-aan, inamalizika kikamilifu na huwa haina uhusiano wowote wa maana au kisarufi na Suwrah inayofuatia. Kisimamo hichi kinatokea pia katika Aayah.

Hukmu yake: Inafaa kusimamiwa na inafaa kuanza kinachofuatia.

الْوَقْفُ التَّامُّ Al-Waqf At-Taamm (Kisimamo Kilichokamilika)

kimegawanyika sehemu mbili:

i- **الْمُطْلَقُ التَّامُّ Al-Waqf At-Taamm Al-Mutwlaq - Kisimamo Kilichokamilika cha Halisi**

Ni kusimama katika neno lakini hata ukiunganisha na yanayofuatia haiharibu maana.

ii- **الْوَقْفُ التَّامُّ الْلاَزِمُ Al-Waqf At-Taamm Al-Laazim - Kisimamo Kilichokamilika cha Lazima ¹**

Ni lazima kusimama kwani kuunganisha na yanayofuatia kutaharibu maana.

¹ Pia kinaeleweka kwa **الْوَقْفُ الْبَيَانُ Al-Waqf Al-Bayaan (Kisimamo cha kufafanua).**

	<p>الْوَقْفُ التَّامُّ الْمُطْلَقُ</p> <p>Al-Waqf At-Taamm Al-Mutwlaq Kisimamo kilichokamilika cha halisi</p>	<p>الْوَقْفُ التَّامُّ اللَّازِمُ</p> <p>Al-Waqf At-Taamm Al-Laazim Kisimamo Kilichokamilika cha lazima</p>
Alama zake katika Aayah ²	<p>ق</p> <p>Qiylaa Inayokusudia kuonyesha kuwa kisimamo kinapendeza.</p>	<p>م</p> <p>Miymu ndogo yenye mkia mfupi inayokusudia kuonyesha kuwa kisimamo ni lazima</p>
Hukmu yake	<p>Inapendeza kusimama na inaruhusiwa kuanza na kinachokuja baada yake, na pia inajuzu kuunganisha na kinachofuatia ikiwa kuwasilisha huko hakutoharibu maana, ndio maana alama hii inadhihirika pia katika الْوَقْفُ الْكَافِي (al-Waqf al-Kaafiy)</p>	<p>Ni lazima kusimama na kisha kuanza na kinachokuja baada yake; kwani kuiunganisha inapelekea kueleweka maana nyengine isiyokusudiwa.</p>

Mifano ya الْوَقْفُ التَّامُّ الْمُطْلَقُ Al-Waqf At-Taamm Al-Mutwlaq -Kisimamo kilichokamilika halisi:

- Mfano wa kwanza mwishoni mwa Aayah:

² Alama hizo zimebainishwa katika Aayah pekee kwani kisimamo hicho cha الْوَقْفُ التَّامُّ (Al-Waqf At-Taamm) huenda kikakotea katika mwisho wa Aayah lakini ni Sunnah kusimama katika kila Aayah kama ilivyothibiti kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم)

مَلِكِ يَوْمِ الدِّينِ ﴿١﴾ إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٢﴾

((Maaliki [Mfalme] wa Siku ya Malipo)) ((Wewe Pekee tunakuabudu na Wewe Pekee tunakuomba msaada))³

Kusimama katika:

يَوْمِ الدِّينِ ﴿١﴾

Hii ni kauli yenye kuelezea utukufu wa Allaah (سبحانه وتعالى) na ufalme Wake kabla ya kuendelea Aayah inayofuatia yenye kuanza na maudhui nyengine kabisa nayo ni kuthibitisha mkataba baina ya msomaji na Muumba wake.

- Mfano wa pili mwishoni mwa Aayah:

أُولَئِكَ عَلَىٰ هُدًى مِّن رَّبِّهِمْ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١﴾ إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ

((Hao wako juu ya Hidaaya kutoka kwa Mola wao, na hao ndio wenye kufaulu)) ((Hakika wale waliokufuru ni sawa kwao ...))⁴

Kusimama katika:

الْمُفْلِحُونَ ﴿١﴾

Hii ni kauli yenye kutoa habari yenye kuhusiana na Waumini katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى) kabla ya kuendelea katika Aayah yenye kuanza na maudhui nyengine kabisa nayo ni habari yenye kuhusiana na makafiri.

- Mfano katikati ya Aayah:

³ Al-Faatihah (1: 4-5)

⁴ Al-Baqarah (2: 5-6)

لَقَدْ أَضَلَّنِي عَنِ الذِّكْرِ بَعْدَ إِذْ جَاءَنِي ۗ وَكَانَ الشَّيْطَانُ لِلْإِنْسَانِ خَذُولًا ﴿٥﴾

((“Kwa yakini amenipoteza mbali na dhikri (ukumbusho na mawaidha) baada ya kunijia.” Na shaytwaan daima kwa insani ni mwenye kusaliti))⁵

Kusimama katika:

إِذْ جَاءَنِي ۗ

hii ni kauli iliyokamilika maana yake, kauli ya dhalimu anaejilaumu nafsi yake na kumlaumu rafiki shaytwaan. Kisha kauli inayofuatia ni kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى) ya kutukumbusha kuhusu maonyo yake kuwa shaytwaan ni khaini (mwenye kusaliti).

Mifano ya الأَوْفَى التَّامِ اللَّازِمِ Al-Waqf At-Taamm Al-Laazim - Kisimamo kilichokamilika cha lazima)

- Mfano wa kwanza mwishoni mwa Aayah:

وَكَذَلِكَ حَقَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ عَلَى الَّذِينَ كَفَرُوا أَنَّهُمْ أَصْحَابُ النَّارِ ﴿٦﴾ الَّذِينَ تَحْمِلُونَ

الْعَرْشَ وَمَنْ حَوْلَهُ يُسَبِّحُونَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَيُؤْمِنُونَ بِهِ ۖ وَيَسْتَغْفِرُونَ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا ...

((Na hivyo ndivyo lilivyothibiti neno la Mola wako juu ya wale waliokufuru kwamba wao ni watu wa Motoni.)) ((Wale (Malaika) wanaobeba 'Arsh na walio pembezoni mwake, wanasabbih kwa Sifa njema za Mola wao, na wanamwamini; na wanawaombea maghfirah wale walioamini ...))⁶

Kusimama katika:

أَصْحَابُ النَّارِ ﴿٦﴾

Kauli hiyo inawahusu makafiri kwamba wao ni watu wa motoni. Kisha inayofuatia ni kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى) Anayotaja Malaika wanaobeba 'Arshi Yake na wanaowaombea

⁵Al-Furqaan (25: 29)

⁶Ghaafir (40: 6 -7)

Waumini maghfirah. Msomaji asiposimama huenda ikafahamika kuwa watu wa motoni ni wabebao 'Arshi.

- Mfano wa pili mwishoni mwa Aayah:

الَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ سِرًّا وَعَلَانِيَةً فَلَهُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٦٧﴾ الَّذِينَ يَأْكُلُونَ الرِّبَا

((Wale ambao wanatoa mali zao usiku na mchana, kwa siri na kwa dhahiri; watapata ujira wao kwa Mola wao, na wala hakuna khofu juu yao na wala wao hawatohuzunika)) ((Wale ambao wanakula ribaa...))⁷

Kusimama katika:

وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٦٧﴾

Kauli hiyo inawahusu Waumini wanaotoa mali zao katika njia ya Allaah (سبحانه وتعالى) kwamba hawatokuwa na khofu wala hawatohuzunika. Kisha inayofuatia inawahusu wenye kumuasi Allaah (سبحانه وتعالى) kuhusu ribaa. Msomaji asiposimama, huenda ikafahamika kwamba wanaokula riba ndio hawatakuwa na khofu wala kuhuzunika.

- Mfano wa kwanza katikati ya Aayah:

وَلَا تَحْزَنْكَ قَوْلُهُمْ إِنَّ الْعِزَّةَ لِلَّهِ جَمِيعًا هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٦٥﴾

((Na wala isikuhuzunishe kauli yao. Hakika taadhima zote ni za Allaah Pekee. Yeye Ndiye As-Samiy'ul-'Aliym (Mwenye kusikia yote daima – Mjuzi wa yote daima))⁸.

Kusimama katika:

قَوْلُهُمْ

⁷ Al-Baqarah (2: 274-275)

⁸ Yuwnus (10: 65)

ili iweze kufikia kutofautisha baina ya kauli mbili; ya kwanza inamuamrisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) asihuzunike wala asishughulike na wasemayo makafiri kwa vile neno ‘qawluhum’ lina maana ‘kauli yao’ (wasemayo). Kisha kauli inayoendelea ni ambayo inathibitisha kuwa utukufu wote ni Wake Allaah; hivyo basi msomaji asiposimama, itafahamika kwamba hiyo ni katika kauli yao makafiri kwamba wanasema: “**Hakika taadhima zote ni za Allaah Pekee**”.

- Mfano wa pili katikati ya Aayah:

لَقَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ فَقِيرٌ وَنَحْنُ أَغْنِيَاءُ سَنَكْتُبُ مَا قَالُوا ...

((Kwa yakini Allaah Ameisikia kauli ya wale (Mayahudi) ambao wamesema: “Hakika Allaah ni fakiri na sisi ni matajiri.” Tutayaandika waliyoyasema...))⁹

Kusimama katika:

وَنَحْنُ أَغْنِيَاءُ

Kauli iliyotangulia yenye utovu wa adabu wa hali ya juu ni ya Mayahudi wasemao kuwa ‘Allaah ni fakiri nao ni matajiri’. Kisha inayoendelea ni kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى) kwamba Ataandika wasemayo. Msomaji asiposimama itafahamika kwamba kauli ya pili ni ya Mayahudi.

⁹ Aal-‘Imraan (3: 181)